

Agrisys Tanzania

Matokeo ya utafiti na warisha



USTAWI WA WAKULIMA

Utafiti ngazi ya kaya ulifanywa katika maeneo ya kilombero kwenye vijiji vya Katurukila, Kidatu, Mang'ula B, Mgudeni, Msalise, Msolwa Stesheni, na Sanje mnamo mwaka 2019. Swali letu lilikuwa, ni namna gani matumizi ya mbinu rafiki kwa mazingira hupellekea kuwa na ustawi wa binadamu?

Ustawi wa binadamu ni nini?



Usalama



Uhuru wa kuchagua na kutenda



Vitu vinavyoashiria maisha bora



Afya



Mahusiano ya Kijamii

Ni nini huboresha ustawi wa binadamu?

- Utumiaji zaidi wa mbinu rafiki kwa mazingira?
 - Kuwa Kijana na mkulima mwanaume
 - Kutumia zaidi pembejeo za viwandani
 - Kuwa na majukumu katika kikundi au katika kijiji
 - Kuwa na mavuno mengi
- Kutumia mbinu rafiki kwa mazingira hasa iliongeza vitu na ustawi wa jamii.

Matumizi ya mbinu rafiki kwa mazingira inajumuisha kutandaza majani, kilimo mseto, kilimo msitu, uvunaji wa maji ya mvua. Wale wanaotambua faida za mazingira na ambao wamepokea zaidi ushauri wa maswala ya kilimo walitumia zaidi mbinu rafiki kwa mazingira.





Ushauri wa maswala ya kilimo hutolewa zaidi na maafisa ugani, mashirika yasiyo ya kiserekali na vyama vya ushrika.


MASHAMBA WANAYOYATAMANI WAKULIMA

Warsha zilifanyika katika vijiji vya Katurukila, Kidatu, Mang'ula B, Mgudeni, Msalise, Msolwa Stesheni, na Sanje mwaka 2021 ili kujua ndoto za wakulima wadogo juu ya mashamba wanayotamani kuwa nayo hapo baadae na kujifunza changamoto na fursa walizonazo.

Wakulima wadogo walitueleza aina ya mashamba wanayoyataka hapo baadae: Ni mashamba **mbalimbali** yenye **mchanganyiko wa mazao ya biashara na chakula, miti na mifugo**. Mazao yanayolimwa ni pamoja na **miwa, mbogamboga na mpunga**. Wanawake hupendelea kupanda mpunga zaidi.



- **Baadhi ya wakulima wadogo wanapendelea miti kuashiria mipaka** au katika **shamba** dogo kwajili ya kuni na mbaao, miti ya matunda na ufugaji nyuki.
- Baadhi wanataka mashamba yao yawe **kando ya barabara na makazi**.
- Baadhi wanapendelea **umwagiliaji** – kutoka kwenye mto, kisima, au mfereji.



MASHAMBA WANAYOTAMANI WAKULIMA

Katika warsha wakulima wadogo waliibuwa changamoto na fursa zinazowakumba;

Wakulima katika warsha walionesha kuwa na hofu kuhusu rutuba ya ardhi, ubora wa mbegu na wadudu katika mazao na magonjwa. Mapendekezo ya kubadili mbinu za kilimo ili kupunguza hizi changamoto yalitolewa na wakulima ikiwa ni pamoja na:



**Matumizi
ya Samadi
na
kupumzisha
shamba**




**Kuacha
magugu kwajili
ya wadudu
maadui wa
wadudu
waharibifu**



**Kuandaa
shamba na
kupanda kwa
wakati**



**Kupanda
mbegu bora
kutoka katika
mamvuno kwa
mwaka
unaofuata**



**Kutumia
vyombo vya
kisasa**

Wakulima **wanapendelea elimu ya maswala ya kilimo** hasa kuhusu udongo na namna ya kutumia pembejeo na **msaada zaidi** kuboresha maisha pamoja kati ya watu na wanyamapori. Pia wanataka kuongeza upatikanaji wa aridhi na mikopo ya riba nafuu.

Wakulima wengi walieleza kuwa na ukosefu wa mitaji. Mapendekezo ya kuongeza mitaji yalikuwa haya:

- Kuunda vyanzo **tofauti tofauti vya mapato**. Kwenye mawazo ya kilimo ilijumuisha: matumizi ya aina mbalimbali za mazao, ufugaji nyuki na upandaji miti kwajili ya mbao na vifaa vya ujenzi. Kupanda mazao ya biashara na mazao ya chakula.

Changamoto za miti katika ardhi zilionyeshwa kama: Muonekano wa shamba wa kutisha kwamba wizi na ajali kutokea pasipo kutambuliwa, vivuli kupunguza mavuno ya mazao na kuzuiliwa matumizi ya kujikusanyia kuni katika maeneo yaliyohifadhiwa:

Mapendekezo yalikuwa:

- Kupanda miti yenye kivuli kidogo katika mpaka wa shamba
- Kuweka miti karibu na nyumbani
- Kuwa na miti mpakani mwa shamba au shamba dogo kwajili ya kuni.

AGRISYS TANZANIA TAARIFA YA MRADI

AGRISYS Tanzania ni mradi (agrisystanzania@gmail.com) wa kutafiti wa faida za kibiolojia na za kiustawi wa maisha ya binadamu zitokanazo na kilimo msitu kwenye mazingira ya kitropiki. Wana shughulika na:

1. Kutambua faida za msingi za kilimo msitu;
2. Kutambua faida za mandhari ya kilimo msitu kwenye shughuli za kilimo;
3. Kutafiti mifumo bora ya kilimo na mchango wake kwenye ustawi wa binadamu.

